



**SWIS-H**  
STATEWIDE INFANT  
SCREENING - HEARING

## MBONA MTOTO WANGU ANAHITAJI KADIRIO YA UCHUNGUZI?

Ikiwa mtoto wako hakupata tokeo wazi kutoka vipimo vya kwanza na pili, atahitaji kadirio ya uchunguzi.

Kutakuwa sababu kadhaa kwa tokeo hilo.

Ingeweza kuwa:

- kulikuwa ugiligili (majimaji) au hali ya kuzuia ndani sikio la mtoto wako baada ya kuzaliwa
- mtoto wako anaweza kuwa na kiasi cha kupoteza uwezo wa kusikia

Ni muhimu kugundua haraka iwezekanavyo jinsi mtoto wako anavyoweza kusikia ili wewe na mtoto wako muweza kupata ushauri sahihi na msaada.

Ukikaa mbali zaidi ya 100 km kutoka hospitali ulipoelekewa, umwombe mtu aliyekupa kifurushi hiki kwa maelezo kuhusu Mpango wa Msaada wa Usafiri wa SWIS-H.

## NINI ITATOKEA KATIKA KADIRIO YA UCHUNGUZI?

Vipimo kadhaa vitafanyikiwa kutoa ujumbe wa makini kuhusu mtoto wako anavyosikia.

Mtaalamu wa kusikia, ambaye ni mtaalamu wa uchunguzi wa uwezo wa kusikia atafanya vipimo. Kadirio hii ni bure bila gharama.

Hakuna kipimo kinachoumiza mtoto wako.

## JE, NIMSAIDIE MTOTO WANGU JINSI GANI KUANDAA KWA KADIRIO?

Ni nzuri zaidi kama mtoto wako amelala wakati wa vipimo. Kwa sababu hiyo, itasaidia ukifika mapema kidogo ili kuna nafasi kumlishe mtoto na kumsaidia kulala.

Kama una watoto wengine, tafadhali umpangalie mtu mwingine kuwatumia nyumbani, ili unaweza kukaa na mtoto wako mnamo kadirio. Lazima mazingira yawe kimya.

Kwa sababu kadirio ya uchunguzi ni pamoja na vipimo anuwai, panga muda wa asubuhi au mchana mzima kutegemea miadi yako imepangiliwa. Unaweza pia kumleta mtu mwingine nawe kukusaidia.



## JINSI GANI KADIRIO YA UCHUNGUZI ITAVYOFANYIKIWA?

Kadirio hii ya uchunguzi inaitwa kipimo cha Kujibu Shina Bongo ya kusikia. Vifaa vya kufahamu vinavyofanana na vile vilivyotumiwa katika uchunguzi vitawekwa kichwa cha mtoto wako. Sauti zitacheza kupitia chombo cha kusikilizia kwa mtoto wako. Majibu ya mtoto wako kwa sauti yatarekodiwa. Majibu haya yanaonyesha sauti ya chini sana kwamba mtoto wako anaweza kusikia.

## NINI ITATOKEA BAADA YA KADIRIO?

Mtaalamu wa kusikia ataweza kukueleza matokeo na kueleza maana ya matokeo, kwa kawaida siku ileile.

Kama mtoto wako anagunduliwa kuwa na kupoteza uwezo wa kusikia, mtapelekwa kwa huduma za maalum pale mmojawapo wa hospitali tatu za watoto katika NSW. Taarifa itatumiwa kwa huduma hizi. Pia nakala itakutumia kwako, daktari wako wa eneo na daktari wa watoto wa mtoto wako na ruhusa yako. Mtaalamu wa kusikia na Mfanyakazi wa Ustawi wa Jamii watakusaidia kupata huduma na msaada ambazo wewe na mtoto wako muweza kuhitaji.

Kama mtoto wako anagunduliwa anasikia kawaida lakini katika hatua ya baadaye unahangaika kuhusu kusikia na maendeleo ya matamshi au lugha ya mtoto wako, tafadhali upange kurudia kupima kusikia wa mtoto wako tena.

Kuongea na daktari wako wa familia ni mahali pazuri pa kuanzia. Uwezo wa kusikia unaweza kupimwa umri wowote.

### KWA MAELEZO Zaidi TAFADHALI UANGALIE TOVUTI IPO CHINI:

<http://www.health.nsw.gov.au/kids-families>

Habari za miadi/wasiliano wa eneo

Kwa ushauri wa afya wasiliana na *healthdirect Australia*

<http://www.healthdirect.gov.au/>

1800 022 222

© NSW Health September 2016 SHPN (NKF) 150243

